

Fred Hutchinson Cancer Center
University of Washington

Fomu ya Ridhaa ya Muda ya Kushiriki katika Utafiti

Nambari ya Itifaki: _____

Jina la Mpelelezi Mkuu: _____

Kama wewe unahudumu kama mwakilishi aliyeamrisha kisheria, mlezi, au unatoa ruhusa ya wazazi kwa mtoto katika utafiti huu, maneno "wewe" na "wako" yanarejelea mtu ambaye unatolea idhini au ruhusa ya kimzazi.

Unaulizwa kujiunga na utafiti. Unapaswa kuchukua muda wako wakati wa kuamua kama utajiunga na utafiti. Unaweza kujadili chaguo zako na mtu yeyote unayetaka.

Kabla ya kuamua ikiwa ungependa kushiriki au la, tutaeleza:

1. Maelezo muhimu kuhusu kwa nini ungependa au hungependa kushiriki katika utafiti;
2. Kwa nini utafiti unafanywa; ni nini kitafanyika wakati wa utafiti, na muda ambao utafiti huu utafanywa;
3. Ni taratibu gani zinazojarihiwa;
4. Hatari na faida zinazotazamiwa ukijiunga na utafiti;
5. Shughuli nyingine zinazoweza kuwa na manufaa badala ya kushiriki utafiti huu; na
6. Jinsi faragha na usiri wako utakavyolindwa.

Wakati husika pia tutakueleza:

1. Nani anayelipia matibabu kama utajeruhiwa wakati wa utafiti;
2. Nafasi ya hatari ambayo hatujui bado;
3. Kwa nini unaweza kuondolewa kwenye utafiti;
4. Gharama yoyote ya kushiriki katika utafiti;
5. Kitakachofanyika kama utaamua kuondoka kwenye utafiti;
6. Wakati utakapojifunza kuhusu matokeo mapya kuhusiana na utafiti;
7. Ni watu wangapi wamepangiwa utafiti;
8. Jinsi maelezo yako na sampuli za mwili (kama vile damu au tishu) zitatumika kwa utafiti huu na utafiti wa baadaye, na kama utapokea mapato yoyote yanayozalishwa kutokana na bidhaa zilizotengenezwa kwa kutumia sampuli za mwili wako;
9. Kama uainishaji wa jenomi nzima unaweza kufanyiwa sampuli za mwili wako;
10. Kama utapewa matokeo ya utafiti uliofanyiwa mwili au afya yako; na
11. Tafiti zozote za hiari ambazo huenda utaombwa kushiriki.

Pia, ikiwa utafiti unahitaji kuchapishwa kwenye [clinicaltrials.gov](http://www.clinicaltrials.gov), tutakueleza:

Maelezo ya jaribio hili la kliniki litapatikana katika <http://www.ClinicalTrials.gov>, kama inavyohitajika na Sheria ya Marekani. Tovuti hii haitajumulisha maelezo ambayo yatakutambulisha. Kwa kiasi kikubwa, Tovuti itajumulisha muhtasari wa matokeo. Unaweza kutafuta kwenye Tovuti hii wakati wowote.

Haki zako

Sio lazima ujiunge na utafiti huu. Uko huru kusema ndio au la. Ikiwa utajiunga na utafiti huu, sio lazima ukae kwa utafiti. Unaweza kuacha wakati wowote (hata kabla ya kuanza). Hakuna adhabu kwa kusema la au kuacha. Huduma yako ya afya ya mara kwa mara haitabadilika.

Ikiwa utakuwa mgonjwa au utaumia katika utafiti, hautapoteza haki yoyote ya kisheria kutafuta malipo kwa kutia saini fomu hii.

Ikiwa utakubali kujiunga, utapata nakala ya fomu hii na nakala ya fomu ya ridhaa katika lugha ya Kiingereza ya utafiti wenyewe.

Kwa maelezo zaidi

Unaweza kuwasiliana na mtafiti mkuu _____ katika _____ wakati wowote una maswali kuhusu utafiti au majeraha yanayohusiana na utafiti.

Unaweza pia kuwasiliana na Mkurugenzi wa Institutional Review Office katika Fred Hutchinson Cancer Center, kwa simu 206.667.5900 au kupitia barua pepe kwenye irodirector@fredhutch.org, kama una maswali kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti.

Saini

Ikiwa utaweka fomu hii sahihi, inamaanisha kuwa tumekuelezea utafiti, na umekubali kushiriki kwa hiari yako.

Jina la Mshiriki Lililochapishwa na Saini au Mwakilishi
Aliyeidhinishwa Kisheria, kama inahusika

Tarehe

Uhusiano wa Mwakilishi Aliyeidhinishwa Kisheria kwa Mshiriki, kama inahusika

Jina Lililochapishwa la Mkalimani/Shahidi na Saini

Tarehe